no-burn.org
breakfreefromplastic.org

#Break Free From Plastic

# Kuelekea sehemu ya pili ya mkutano wa majadiliano (Utakaofanyika tarehe 29 Mei hadi Juni 2 jijini Paris Ufaransa), wanachama wa GAIA na BFFP kutoka Afrika watoa wito kwa viongozi wa Afrika kupigania mkataba wa kimataifa wa taka plastiki ulio imara.

Mkataba wa kimataifa wa taka plastiki unaipa Afrika fursa ya kihistoria ya kushughulikia changamoto za kipekee ambazo bara linakabili kutokana na athari mbaya za uwepo wa mifumo ya plastiki. Katika kikao chake cha kwanza, kamati ya majadiliano ya mkataba huu (INC1), iliomba sekretarieti kuandaa, kwa kuzingatiwa makubaliano ya kamati kuelekea kikao chake cha pili, hati yenye vipengele vya msingi vitakavyosaidia kupata mkataba wa kimataifa unaofungamanisha kisheria, kwa kuzingatia uwasilishaji wa **nchi zilizo sehemu ya mkataba ambapo nchi 14 za Kiafrika ziliwasilisha mapenedekezo binafsi ukiachana na mapendekezo jumuishi juu ya malengo ya msingi; majukumu ya msingi, hatua za kudhibiti na kutekeleza mambo kwenye mkataba huu wa plastiki wa kimataifa.**

Izingatiwe, mapendekezo jumuishi ya Afrika yalisisitiza wazi juu n kuu ya **kumaliza uchafuzi wa plastiki kupitia kupunguza uzalishaji wa plastiki na matumizi.** Msimamo mkali wa Afrika katika kushughulikia uchafuzi wa plastiki kuanzia kwenye mzunguko wa maisha yake ambayo ni muhimu kwa ajili ya kulinnda uhuru wa Afrika hasa kwa sababu bara hili linaendelea kubeba mzigo wa taka plastiki kutoka nje zenye sumu na zisizoweza kuchakatwa kwa njia ya ukoloni wa taka. Huu ni msimamo ambao mataifa yote ya Afrika yanapaswa kupitisha kama mlengo wa lazima katika mkataba huu wa plastiki.

Nchi tano zinatawala uzalishaji wa mafuta barani Afrika, orodha hii inaweza kuongezeka kwa sababu ya miradi mipya ya uzalishaji wa mafuta na gesi. Nchi nyingi kati ya hizo hutawala pia matumizi ya plastiki, uagizaji wa kemikali na zinchafuzi pamoja na **kuwa na historia ya kutengeneza faida ya faida kwa uharibifu wa maisha ya watu.** Fursa hii muhimu ya kupunguza athari zitokanazo na uchafuzi wa taka plastiki iko katika hatari ya kudhoofishwa na nguvu na ushawishi kutoka kwenye sekta ya plastiki, kinyume na haki za msingi za binadamu za jamii zilizo katika mazingira hatarishi kama waokota taka wasio rasmi. Uwasilishaji kwenye (INC2) kutoka nchi kama kumeonesha hari ya chini na ushawishi wa masuluhisho ya uongo kama vile kuchoma taka, kuchakata kemikali, plastiki kwa michakato ya mafuta au plastiki-kwa-kemikali, pyrolysis na gesi ambayo ina uwezo wa kuunda athari kali za kiafya kwa wafanyakazi, jamii na mazingira kwa kutoa viwango vya juu vya gesi chafuzi, uchafuzi wa hewa yenye sumu, majivu yenye sumu, na mabaki mengine hatari.

Kadhalika, **Afrika imekuwa ikiongoza njia katika mapambano dhidi ya taka plastiki,** ikiwa nchi 34 za Kiafrika zimepitisha sheria zinazopiga marufuku vitu vya plastiki ili kuzuia masilahi hasi ya kiuchumi na kibinafsi ya kampuni za kemikali na faida kuwekwa mstari wa mbele dhidi ya watu, mazingira na afya ya binadamu. Kama ilivyotamkwa na muwasilishaji maalum kutoka Umoja wa Mataifa, ni muhimu mkataba huu kuwa **"mlengo unaothamini haki za binadamu ikija kwenye usimamizi wa mambo yanayohusisha plastiki duniani, ukizingatia kanuni za haki za binadamu, mifumo ya uwajibikaji na upatikanaji wa suluhisho".**

**Tatizo la taka plastiki limeendelea kuongeza ukosefu wa haki unaosababishwa na ukoloni, utumwa, ubaguzi wa rangi na ubepari ambao unazidi mipaka yetu ya sayari,** na unaumiza vibaya jamii za kipato cha chini na haswa watu weusi na makundi ya kiasilia.

Inanyima wachukuzi wa taka haki yao ya kupata maisha salama na kipato cha haki. Mawasilisho kwenye INC2 kutoka nchi zingine za Afrika yameshindwa kuafiki jukumu muhimu la wachukuzi wa taka. Ni wazi kuwa wachukuzi wa taka ni uti wa mgongo wa mifumo ya ukusanyaji wa taka na mifumo ya uchakatji kwa hivyo, **waokota taka wanastahili kutiliwa msisitizo katika mkataba huu mpya wa plastiki,** ili kuhakikisha ujumuishaji wao wenye maana katika vifungu vya makubaliano na utekelezaji wa mkataba, utakao wajengea uwezo wao zaidi kama wahandisi wa uchumi wa rasilimali za ulimwengu, utakaowaweka kwenye kiini cha mfumo mzima wa ukusanyaji, utenganisho, ukarabati, uzalishaji wa mbolea na mifumo ya kuchakata tena ya taka.

**Sisi, kama wanachama wa GAIA na BFFP barani Afrika tunaowakilisha sekta ya asasi zisizo za kiserikali kutoka Tanzania, Kenya, Ghana, Nigeria, Afrika Kusini, Gambia, Mauritius, Tunisia, Uganda, Cameroon, Misri, Ethiopia na DR Congo tunatoa rai kwa wasimamizi wa nchi kwenye INC kutoka Afrika, tukiwaomba wazigatie mapendekezo yafuatayo:**

- **Msimamo imara unaounga mkono mapendekezo jumuishi ya Afrika juu ya kupunguza biashara, uzalishaji na utumiaji wa plastiki,** kupunguza uwepo wa kemikali zenye sumu katika plastiki, kukataza vitendo hatarishi kama vile kuchoma moto taka, matanuru, shughuli za kuwasha moto kwenye mitambo ya makaa ya mawe na michakato mingine ya taka-kwa-nishati, usindikaji kwenye viwanda vya saruji, na kuchakata kemikali ili kulinda afya ya binadamu na mazingira.

- **Kuzingatiwa kwa makubaliano ya haki za binadamu ya Umoja wa Mataifa** juu ya kuwa na mazingira safi, salama na yenye afya.

- **Hakika ya ujumuishaji wa haki kwenye kipindi hiki cha mpito kwa wachukuzi wa taka na jamii kutoka mazingira hatarishi,** ili wapewe nafasi kwenye mchakato wa sera za usimamizi wa taka za kitaifa na wa Mkataba wa kimataifa wa plastiki.

- **Utekelezaji na uimarishaji wa sheria zilizopo juu ya matumizi ya plastiki za mara moja na zile zinazoharibu mazingira** ndani ya nchi za jumuiya ya Afrika.

- **Kutambua kuwa vitendo vya usimamizi wa taka peke yake havishughulikii athari kamili kwenye mifumo ya plastiki, na kwamba kuchakata ni muhimu sana kama kutaondoa uzalishaji wa plastiki asili,** badala ya kutumia plastiki kuchakata bidhaa ambazo zilitengenezwa kutoka kwenye vitu asilia ( mfano: katika nguo).

- **Kupinga masuluhisho ya uongo** kama vile plastiki zinazoweza kuharibika na zinazotumika kutengenezea mbolea, mifumo ya uchomaji taka na plastiki au uchomaji wa plastiki katika viwanda vya saruji ).

- **Kuimarisha na kukuza masuluhisho endelevu ndani ya bara** kama vile mfumo wa taka sifuri na urejelezi.

- **Kupinga mifumo ya kifedha ambayo inakuza uzalishaji wa plastiki unaoenea na kusaidia kuendela kuchafua mazingira,** kama vile mikopo ambayo inaruhusu mashirika ya kimataifa kukwepa majukumu yao ya kifedha, kisheria kimaadili juu ya shida ya plastiki wanayosababisha. Vilevile, kupinga mashirika haya kufanya kidogo au kukwepa kabisa tatizo na ufadhili wao kuelekea mabadiliko ambayo ni ya haki.

- **Anzisha vigezo vya ufanisi, miradi rafiki kwa mazingira inayoongozwa na serikali na sio wazalishaji na waunga mkono uzalishaji wa plastiki.** Kuwe na malengo ya wazi yanayojumuisha wadau wote kwenye jamii wa sekta za uchakataji na urejelezi.

- **Pitisha mikakati inayoendana na vithibitisho vya maamuzi vya kisayansi** na kama msingi wa mchakato wote wa Mkataba huu wa Plastiki.

- **Kuwezesha utekelezaji mzuri wa mkataba huu kupitia mifumo mizuri ya fedha, teknolojia ambayo ni rafiki kwa mazingira** na sio ya zamani na kujenga uwezo kwa vikundi vyote husika katika mfumo wa plastiki.

Tunasisitiza na kutilia mkazo tena kwamba kupunguza uzalishaji wa plastiki kwenye chanzo bado ni sehemu ya msingi ya juhudi za kupunguza uzalishaji wa gesi chafu, kujenga uimara wa mifumo ya jamii na suluhisho la tatizo la mabadiliko ya tabia ya nchi kwa namna ya haki, na usawa kwa wote.